Uchanganuzi wa Ufaafu wa Tafsiri ya Ombi la *Baba Yetu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili

Virginia Mwathi[1], Larry Ndivo[2]
[1]Chuo Kiku u cha Laikipia, Kenya
[2]Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya

Ikisiri
Makala hii ilichunguza ufaafu wa tafsiri ya ombi la *Baba Yetu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Watafiti wanashikilia kuwa tafsiri inafaa kuwa na ufanifu mkubwa kuliko udhaifu. Lengo la watafiti ni kudhihirisha ufaafu na udhaifu wa tafsiri hii. Sanaa ya tafsiri ni muhimu sana katika ulimwengu wa sasa. Imewezesha mawasiliano ya kimataifa hasa katika elimu, biashara na shughuli za kidiplomasia. Watafiti wanakubali kuwa mchakato wa tafsiri huathiriwa na vizuizi kama vile vya kitamaduni na kimuktadha na hata tofauti za kisarufi katika lugha tofauti. Katika makala hii, matini asili na matini lengwa zilisomwa, vipengele vya ufaafu na udhaifu kudondolewa kisha watafiti kutoa msimamo wao wakiongozwa na mkabala wa House (1977 & 2015) kuhusu ubora wa tafsiri na pia nadharia ya Tafsiri ya Kimawasiliano ya Newmark. Walipata matokeo ya utafiti huu kama kuhifadhiwa kwa maana katika matini lengwa. Usawa wa kikazi unaopendekezwa na House ulidhihirika na pia usawa wa kimawasiliano unaozungumziwa na Newmark ulijitokeza. Utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa wanafunzi, wahadhiri na wasomi wengine katika uwanja wa tafsiri kwa vile utakuwa rejeleo muhimu katika kazi za tafsiri. Kwa kufanya hivi, watafiti wanaamini kuwa tafsiri sahihi ni kichocheo katika mafanikio ya mawasiliano.

Istilahi muhimu: Makala Asili, Makala Lengwa, Tafsiri, Udhaifu, Ufaafu

Abstract
This paper examined the appropriateness of translating the Lord's Prayer from English into Kiswahili. The researchers maintain that an effective translation should exhibit more strengths than weaknesses; thus, this study aims to delineate both the appropriate dimensions and the limitations of the translated text. In today's globalized world, translation plays a vital role in facilitating international communication, particularly in educational, commercial, and diplomatic spheres. However, researchers agree that the translation process is usually affected by barriers, including cultural and contextual ones, as well as grammatical differences between languages. In this article, the researchers read the source and target texts, identified strengths and weaknesses, and then took their stand guided by House's approach to translation appropriateness and Newmark's Communicative Translation Theory. The findings showed that the target text retained meaning, achieved the functional equivalence proposed by House, and met the communicative function proposed by Newmark. This research will be important to students, lecturers, and other scholars in the field of translation, as it will serve as a reference for translation work. Ultimately, these findings reinforce the premise that accurate translation serves as a critical facilitator of successful intercultural communication.

Keywords: Appropriateness, source text, target text, translation, weakness

Utangulizi

Taaluma ya tafsiri imekuwa muhimu sana hasa katika ulimwengu huu wa uwingi lugha kutokana na kutangamana kwa watu watokao katika tamaduni tofauti zenye lugha tofauti. Wataalam kadhaa wamefafanua maana ya tafsiri wakiwemo, Catford (1965) anayesema kuwa tafsiri ni kubadilisha maandishi kutoka lugha asili na viwakilishi vya maandishi hayo katika lugha lengwa. Newmark (1988) anashadidia kwa kusema kuwa tafsiri ni sanaa inayojumuisha jaribio la kuhawilisha ujumbe ulioandikwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Munday (2016) naye anasema kuwa tafsiri ni mchakato wa kubadilisha matini andishi kutoka kwa lugha asili kwenda kwa lugha lengwa. Mchakato huu huongozwa na mtafsiri katika muktadha maalum wa kijamii na kitamaduni. Munday anaendelea kueleza kuwa makala asili (M.A) ni matini asili inayotafsiriwa katika lugha asili (L.A) ilhali makala lengwa ni zao la mwisho; toleo lililotafsiriwa katika lugha lengwa (L.L). Ifahamike kuwa, M.A si lazima iwe ndiyo muundo asili. Inaweza kuwa pia ni tafsiri ya makala nyingine, hasa katika tafsiri isiyo ya moja kwa moja.

Kabla ya kuhakiki ufaafu wa tafsiri katika matini teule, ni vyema kung'amua kuwa tafsiri ina umuhimu mkubwa. Hufanya jukumu muhimu sana katika kufanikisha mawasiliano katika mipaka ya kiisimu na kitamaduni. Utandawazi unavyozidi kuongezeka, uwezo wa kupitisha mawazo, habari na hisia kwa lugha nyingi umekuwa muhimu kwa kukuza uelewano na ushirikiano miongoni mwa jumuiya tofauti. Pym (2010) anasema tafsiri ni muhimu katika ufanisi wa biashara na diplomasia kwa vile huhakikisha uwazi na kujenga imani na washikadau wa kigeni. Venuti (2012) anasema kuwa tafsiri inawezesha uhifadhi na usambazaji wa utamaduni na fasihi. Inatajirisha fasihi ya ulimwengu kwa kufanya kazi ya fasihi kupatikana hata nje ya jamii zao asili za kiisimu. Cronin (2013) naye anadokeza kuwa tafsiri inawezesha upataji wa habari kwa usawa katika ulimwengu wa uwingi lugha. House (2015) anashadidia kwa kusema kuwa tafsiri haihusu tu ubadilishaji wa kiisimu bali pia ni daraja la kitamaduni linalosaidia kudhihirisha muktadha, toni na makusudio kati ya tamaduni anuwai.

Erton (2020) ameeleza kwa upana kuhusu stadi na uwezo wa mtafsiri au msomaji. Ni muhimu kuwa na stadi hizi ili kufanya na kuhakiki kazi ya tafsiri kikamilifu. Katika makala hii, tulihakiki matini tafsiri teule kama msomaji. Yaani, tulichukua nafasi ya msomaji kwa vile tafsiri yenyewe ishafanywa. Uwezo na stadi kuu alizoeleza Erton ni pamoja na utaalam. Erton (2020) akimnukuu (Arsoy, 2020), anadai kuwa wenye sifa hii ya utaalamu ni waaminifu katika tabia zao za kibinafsi. Hivyo husawiri sifa ya kuwa kielelezo bora kwa wengine. Licha ya kuwepo kwa maoni kinzani, wao hushughulikia kila mtu kwa usawa bila kubagua. Katika makala hii, watafiti walitumia utaalam huu kuhakiki ufaafu wa tafsiri teule. Hivyo, ilitarajiwa kuwa uhakiki na matokeo ya utafiti yangekuwa yenye usawa. Erton (2020) anadokeza vitabia vya utaalam. Hivyo ni: nidhamu, subira, usawa, usiri, upangaji na ufanyaji wa kazi kwa wakati unaofaa. Uzingatiaji wa haya humtunuku mtaalam nafasi spesheli katika taaluma hii ya tafsiri katika jamii. Mtafsiri anafaa kuwa mkweli yaani, awe mwaminifu na asitawaliwe na maoni ya kibinafsi, hisia na udhaifu wowote. Awe mnyenyekevu na mwenye nia ya kutaka kujua au kusoma, kuimarika, kubadilika na kujijua.

Arslan (2010) katika Erton (2020) anadokeza stadi nyinginezo kama vile kuwa na maarifa ya hivi sasa ili kazi ya tafsiri kufanyika na kueleweka kulingana na matukio ya wakati uliopo. Anaendelea kudokeza stadi nyingine ambayo ni ujuzi na ufaafu katika matumizi ya sarufi. Anasema kuwa ujuzi wa lugha ya mama na lugha ya kigeni husaidia katika kujieleza katika majukwaa tofauti ya kitaalam na kijamii na hivyo kutoa nafasi bora katika kutafsiri na kufasiri.

Watafiti walikubaliana na dai hili kwa vile ni kweli kuwa huwezi ukatafsiri kazi bila kuwa na umilisi wa sarufi ya lugha ya matini asili na matini lengwa. Erton (2020) anaongeza stadi nyingine ambayo ni ujuzi wa maisha ya jamii na utamaduni wake. Watafiti walikubaliana naye kwa kuchangia kuwa ujuzi huu wa utamaduni wa lugha asili na lugha lengwa utamwezesha mtafsiri kupata viwakilishi vya lugha asili katika lugha lengwa vinavyooana na utamaduni wa lugha lengwa na hata kukubalika katika utamaduni huo. Zaidi ya yote, watafiti walishikilia kuwa msomaji anapokuwa na stadi zilizoelezwa, atahakiki kazi ya tafsiri kwa uwazi bila ubaguzi. Watafiti wanadokeza kuwa wana umilisi wa sarufi na utamaduni wa lugha asili na lugha lengwa za matini teule. Kwa hivyo wana uhakika kuwa uhakiki watakaoufanya utakuwa wenye utaalam.

Suala la Utafiti

Bila tafsiri, ujumbe muhimu ungekosa kufikia walengwa. Hii ni kwa sababu tafsiri ni sanaa muhimu katika ulimwengu huu wa uwingi lugha. Ni daraja la kitamaduni ambalo linawezesha mawasiliano kati ya watu wanaozungumza lugha tofauti. Hii ni hasa katika nyanja za elimu, biashara, diplomasia na kadhalika. Tangu kuvumbuliwa kwa sanaa hii, tafsiri nyingi zimefanywa katika fasihi, biashara. elimu, afia na kadhalika. Kando na kuwezesha ubadilishanaji wa maarifa, watafiti wanaamini kwamba tafsiri hizi hazikosi ufaafu na udhaifu. Hivyo katika utafiti huu, watafiti walihakikiki tafsiri ya Ombi la *Baba Yetu* ili kubaini ufaafu na udhaifu wa tafsiri hii.

Misingi ya Nadharia

Katika kuhakiki ufaafu wa tafsiri ya ombi la *Baba Yetu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, watafiti waliongozwa na mtazamo wa House (1977 & 2015) kuhusu ubora wa tafsiri. House (2015) anaona tafsiri kama tendo la kimawasiliano ambapo kazi ya matini katika L.L inafaa kulingana kwa karibu na matini ya L.A. Anadai kuwa tafsiri husemekana kuwa faafu ikiwa inahifadhi maana ya kipragmatiki na ulinganifu wa kikazi wa M.A. Yaani, M.L ifanye kazi sawa na M.A katika na kulingana na muktadha wake wa kitamaduni na kiisimu. Anaamini kuwa tafsiri huwa fanifu ikiwa inaumba athari sawa za kimawasiliano kwa hadhira zao. Mnamo mwaka wa 2015, alikuza modeli ya kutathmini ubora wa tafsiri, ambapo ufaafu hutathminiwa kulingana na namna tafsiri inavyozaa upya kazi ya M.A katika mazingira yake mapya ya kiisimu na kitamaduni. Kwa hivyo, ufanisi wa tafsiri si wa kiisimu tu bali pia kimuktadha na kitamaduni.

Katika modeli ya kutathmini ubora wa tafsiri, House (2015) anazungumzia yafuatayo: kwanza, ni semantiki ambapo uteuzi wa kileksia, misemo na sitiari huangaliwa kudhibitisha kuwa zote zimetumika kuhifadhi maana ya M.A. Pili ni pragmatiki ambapo maana inayokusudiwa pamoja na matendo kauli huangaziwa. Kumaanisha kuwa si usemi tu hutazamwa bali ni maana inayokusudiwa na usemi huo. Kwa hivyo katika tafsiri, mtafsiri atazingatia maana inayokusudiwa na usemi bali si kufanya tafsiri ya moja kwa moja. Tatu ni umatini ambapo mshikamano katika kazi na kueleweka kwake huangaziwa. Yaani, kazi ya M.L iwe na dhana zinazoshikamana na hivyo kuzaa maana inayoeleweka kuambatana na M.A. Mwisho ni umuktadha. Hapa ni namna vipengele vya kihali vinavyohifadhiwa katika M.L. Vipengele vya kihali vilikuwa vimezungumziwa hapo awali na House (1977). Vipengele hivi ni: nyanja ambayo huhusu mada inayozungumziwa. Pili ni wahusika na mahusiano yao na mwisho ni njia ya mawasiliano. House anadai kuwa haya yote sharti yazingatiwe katika kutathmini ubora wa tafsiri na sharti yahifadhiwe katika M.L.

Mtazamo wa House ulishadidiwa na nadharia ya tafsiri ya kimawasiliano ya Newmark (1988 & 1991). Mihimili mikuu ya nadharia hii iliyoongoza watafiti ni: kwanza, tafsiri ya kimawasiliano inampa msomaji kipaumbele. (Nida na Taber, 1992) wanasema ufaafu wa tafsiri unafaa

kuchunguzwa kwa kuzingatia kiwango cha uelewa wa msomaji wa kawaida, ambaye analengwa na tafsiri fulani, atakavyouelewa ujumbe ipasavyo. Pili, inalenga kuleta athari sawa kati ya msomaji wa matini asili na yule wa matini tafsiri. Mambo yatakayokwaza uwepo wa athari sawa hudondolewa. Katika suala hili la kuleta athari sawa kwa hadhira ya matini asili na lengwa, watafiti walielewa hili kama, kutopotoka kwa maana. Hivyo, maana katika M.A idumishwe katika M.L. Tatu, nadharia ya tafsiri ina uaminifu kwa msomaji na ni huru. Yaani, mtafsiri ana uhuru wa kutafuta visawe vya karibu iwezekanavyo, kuondoa utata, kudondosha sehemu fulani za matini na kuondoa urudufu. Watafiti walihitilafiana na suala la kudondosha sehemu fulani za matini na pia kuondoa urudufu kwa kuuliza je, haya mawili hayataathiri maana? Je, urudufu una makosa gani hivi kwamba mtafsiri ana uhuru wa kuuondoa? Kwa kawaida, tunajua kuwa uradidi huleta dhana ya kusisitiza. Je, urudufu ukiondolewa, lengo la kusisitiza litapatikana katika M.L?

Mbinu za Utafiti

Utafiti ulikuwa wa maktabani. Matini teule ziliteuliwa kwa usampuli wa kimakusudi kwa vile watafiti walikuwa na lengo maalum la kuhakiki kazi za tafsiri. Hivyo, walibidiika kutafuta makala ambayo ni tafsiri. Pamoja na hayo, watafiti ni Wakenya wenye umilisi wa lugha mbili rasmi ambazo ni Kiingereza na Kiswahili. Hivyo, kulikuwa na imani kuwa wangehakiki kazi hizi kulingana na utaalam uliopendekezwa hapo awali na Erton (2020).

Historia Fupi ya Ombi la *Baba Yetu*

Ombi la *Baba Yetu* (*The Lord's Prayer au Our Father*) ni moja ya maombi yanayojulikana sana na kukaririwa mara kwa mara na Wakristo. Asili yake inaweza kufuatiliwa moja kwa moja kwa Yesu Kristo ambaye kulingana na Agano Jipya, alifunza wanafunzi wake kule mlimani (Mathayo 6:9-13). Ombi hili linadhihirika pia kwa ufupi katika kitabu cha Luka 11:2-4. Vifungu hivi vinafanya jukumu la kuwa matini msingi kwa matumizi ya ombi hili katika liturujia na ibada ya Kikristo (Pelikan, 2005). Pelikan anaendelea kudokeza kuwa kihistoria, ombi hili liliundwa kwa Kiaramu, lugha ya kila siku iliyozungumzwa na Yesu na wenzake lakini likarekodiwa kwa Kigiriki. Hii ni katika miswada asili ya Agano Jipya. Toleo la Kigiriki limekuwa msingi wa tafsiri nyingi zikiwemo toleo la Kilatini linalopatikana Vulgata. Lilitafsiriwa na Mtakatifu Jerome katika karne ya nne baada ya masihi. Ombi hili limefanyiwa tafsiri na fasiri nyingi kadri ya mpito wa karne na kuingia katika miktadha ya kiisimu, kitamaduni na kidhehebu. (Metzger na Ehrman, 2005) wanaeleza kuwa ingawa muundo msingi wa ombi hili unabaki thabiti, tofauti zipo kati ya toleo zinazotumika na tamaduni tofauti za Kikristo. Katika makala hii, watafiti wametumia *Biblia Maandiko Takatifu* kama makala lengwa huku makala asili yakiwa *The Holy Bible- King James Version.*

Matokeo ya Utafiti na Majadiliano

Uhakiki wa Tafsiri ya Ombi la *Baba Yetu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili

The *Lord's Prayer* ni ombi linaloanza kwa kumtambua Mungu kama mzazi wa kiume yaani 'baba' ingawaje katika muktadha wa dini, neno baba lina maana ya mzazi wa kiroho. Utambuzi wa muktadha katika taaluma ya tafsiri ni muhimu. Ni kipengele cha utaalam katika uwanja wa tafsiri kwa mujibu wa Erton (2020). Canale (1983) katika Erton (2020) anadai kuwa umilisi wa kiisimujamii ni muhimu katika tafsiri na mawasiliano. Kulingana naye, umilisi huu unahusu utangamano wa kibinadamu katika miktadha asili; matamshi yanayotolewa na maana yake katika miktadha tofauti ya kijamii na kitamaduni. Watafiti wanakiri kwamba si kila wakati ambapo neno 'baba' huwa na maana ya mzazi. Mzazi anaweza kumuita mwanawe 'baba' labda kumwonyesha

mapenzi, au kumbembeleza ama kama alimpa jina la mzazi wake. Watafiti wakiongozwa na upragmatiki wa House (2015), wameng'amua kuwa neno hili limetumika kurejelea mzazi na hasa wa kiroho kwa vile muktadha wa ombi hili ni wa kidini. Baada ya utambuzi wa Mungu kama baba na kutaja makaazi yake kwa kusema, " *Our Father which art in heaven*..." ombi hili linamtukuza na kuomba utukufu wake uje kwa kusema, "*Hallowed be thy name. Thy kingdom come*..." Kufikia hapo toleo la Kiswahili limedhihirisha haya haya bila kupotosha kwa kusema, "Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje..." Toleo la Kiingereza linaendelea kusema, "*Thy will be done in earth as it is in heaven*..." Tafsiri yake katika Kiswahili ni, 'Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni...' Kufikia hapo, watafiti hawajapata hitilafu yoyote katika tafsiri hii. Inatokea kuwa ya sentensi kwa sentensi. Huu ni mkabala mmojawapo unaopendekezwa na Newmark (1988). Watafiti wanaona kuwa maana katika M.A imehifadhiwa namna ilivyo katika M.L.

Toleo la Kiingereza linaendelea kusema, "*Give us this day our daily bread*..." Ni muhimu kufahamu kuwa katika sentensi hii, kuna suala la maana na utamaduni. Spencer (2002) anadokeza kuwa kwa muda mrefu, mkate umekuwa ndio chakula kikuu cha Waingereza, mara kwa mara kikiambatanishwa na viazi na nyama hasa tangu kipindi cha mapinduzi ya viwanda. Kutokana na dokezo hili, watafiti wanang'amua kuwa neno mkate katika muktadha wa ombi hili likioanishwa na utamaduni wa Waingereza, lina maana ya riziki. Toleo la Kiswahili linasema, " Utupe leo riziki yetu..." Watafiti wakiongozwa na usemantiki wa House (2015), wanaona kuwa katika uteuzi wa kileksia, mtafsiri ameteua sitiari bora (riziki) kusimamia neno 'mkate'. Kwa hivyo kipragmatiki, amedhihirisha maana inayokusudiwa na M.A katika M.L. Hili ni dhihirisho kuwa mtafsiri ameweza kumudu tafsiri hii kwa vile amehifadhi maana katika muktadha wake kwa kutumia neno riziki. Nadharia ya tafsiri ya kimawasiliano ni huru kama tulivyotaja hapo awali. Yaani, mtafsiri ana uhuru wa kutafuta visawe vya karibu katika L.L ili kuondoa utata. Kwa hivyo, matumizi ya neno 'riziki' kusimamia neno 'mkate' ni kisawe cha karibu sana kinachoondoa utata na kuhifadhi maana, dhihirisho la kuwa mtafsiri amemudu kazi yake. Toleo la Kiswahili halijataja 'riziki yetu ya kila siku, dhihirisho la kuwa kuna kupunguka kwa maana. Kwa mujibu wa House (2015) tafsiri ni faafu ikiwa ina mshikamano. Hii ni sifa mojawapo ya umatini katika vipengele vyake vinavyodhihirisha tafsiri faafu. Katika sehemu hii, kupunguka kwa maana kutokana na sehemu fulani kudondolewa katika matini kunadhihirisha kutokuwepo kwa mshikamano; yaani kutiririka na kushikamana kwa dhana ili kuzaa maana inayoeleweka kuambatana na M.A. Kwa hivyo, tukio hili ni mojawapo ya upungufu wa tafsiri hii.

FAO (2021) ni shirika linalodai kuwa mahindi ndiyo chakula kikuu na cha msingi katika jamii nyingi eneo la Afrika Mashariki. Mahindi ndiyo msingi wa vyakula kama ugali, posho ama sima. Ifahamike kuwa, chimbuko la Kiswahili ni Afrika Mashariki na hivyo kuna uhusiano kati ya Kiswahili na utamaduni wa wenyeji wa eneo hili. Hivyo watafiti wanapendekeza kuwa, mtafsiri angetumia neno ugali kusimamia mkate katika toleo la Kiswahili, ingekuwa sawa pia. Hii ni kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya kimawasiliano inayompa mtafsiri uhuru wa kutafuta visawe vya karibu katika M.L na vilevile usemantiki wa House wa uteuzi wa kileksia, misemo na sitiari zitakazofaulisha usawa wa maana na hivyo kuleta athari sawa kati ya hadhira ya M.A na M.L.

Toleo la Kiingereza linaendelea kusema, "...*And forgive us our debts as we forgive our debtors*..." huku la Kiswahili likisema, " Utusamehe deni zetu, kama sisi tuwasamehevyo wadeni wetu..." Katika sehemu hii, kuna suala la maana na muktadha pia. Aidha, usemantiki na upragmatiki ni vipengele vinavyodhihirika .Neno *debtor* kwa kawaida lina maana ya mtu mwenye deni ambalo anafaa kulipa. Lakini katika muktadha huu, kisemantiki na kipragmatiki, linatoa maana ya 'aliyekosa' au 'mwenye dhambi'. Matumizi ya maneno 'deni' na 'wadeni' katika toleo

la Kiswahili linadhihirisha tafsiri ya moja kwa moja. Watafiti wanaona kuwa mtafsiri hajachukua jukumu la kufumbua maana ya '*debtor*' katika M.L kama alivyofanya katika neno '*bread*'. Hii ni kumaanisha kuwa, amekiuka mhimili mmoja wa nadharia teule. Mhimili huu ni ule wa kumpa msomaji kipaumbele kwa maana ya, ufaafu wa tafsiri unafaa kuchunguzwa kwa kuzingatia kiwango kile msomaji wa kiwango cha wastani, ambaye analengwa na tafsiri fulani, atakavyouelewa ujumbe ipasavyo (Nida na Taber, 1992). Kwa hivyo, msomaji wa kawaida wa M.L atakosa kupata maana lengwa ya neno *'debtor'.* Huu ni udhaifu katika tafsiri.

Pamoja na hayo, sentensi hii ya Kiingereza inatokea kuwa na utata kwa vile ina maana mbili. Kwanza, inajitokeza kama sentensi ya kumithilisha. Neno '*as'* lina maana ya kufananisha. Kwa hivyo, maana ya sentensi hii ni kuwa Mungu atuige tunavyowasamehe wanaotukosea. Pili, inatokea kama sharti, yaani, kufanyika kwa jambo moja kunategemea kufanyika kwa jingine. Kwa hivyo dhana inayotokea ni 'tusamehe ili nasi tusamehe waliotukosea'. Toleo la Kiswahili linaonyesha kutochukua utata huu bali limeurekebisha kwa vile maana inayotokea ni moja, ile ya kumithilisha. Matumizi ya maneno 'kama sisi tuwasamehevyo wadeni wetu...' yanatoa dhana ya kumithilisha. Kumaanisha kuwa mtafsiri ametumia uhuru wake uliopendekezwa na Newmark (1991). Uhuru huu ni ule wa kuondoa utata. Kwa hivyo, amemudu tafsiri hii.

Mwisho, Toleo la Kiingereza linasema, "*...And lead us not into temptation, but deliver us from evil*: *For thine is the kingdom, and the power, and the glory, for ever. Amen."* Toleo la Kiswahili limetafsiri hii kama, "Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina." Tafsiri ya neno *evil* ni uovu. Katika toleo la Kiingereza, linajitokeza kama nomino dhahania, yaani ni kitu kisichoshikika. Hudhihirika kupitia kwa matendo mengine. Kwa mfano, kuiba ni tendo ovu. Tunapoangalia toleo la Kiswahili, linasema 'yule mwovu'. Kumaanisha kuwa tafsiri haijachukua ule udhahania uliopo katika M.A. Sasa katika M.L, imetokea kama nomino ya kawaida. Hii inadhihirisha kwamba maana iliyokusudiwa katika M.A haijahifadhiwa katika M.L. Kwa hivyo kisemantiki kwa mujibu wa House (2015), mtafsiri amefeli katika uteuzi wa leksimu mwafaka kusimamia nomino dhahania ambayo ni *evil.*

Baada ya uhakiki huu, watafiti wanadai kuwa tafsiri ya ombi la *Baba Yetu* imefaulu kwa kiwango kikubwa licha ya kuwepo kwa hitilafu kidogo zilizodhihirishwa. Imefaulu kwa vile tunaporejelea mkabala wa House (1977 & 2015) usawa wa kikazi wa toleo hizi mbili unadhihirika. Kimuktadha kwa mujibu wa House, vipengele vya kihali vimehifadhiwa katika M.L. Kipengele cha hali kinachodhihirika ni nyanja. Kwanza, toleo zote mbili zinadhihirika kuwa katika uwanja wa kidini. Pili, zote zinadhihirika kama sifa na ombi. Aidha kipragmatiki, M.L ingali inajitokeza kama sifa na ombi kwa jumla na hivyo imefaulu. Mtafsiri ameweza kudumisha maana kwa kiwango kikubwa kutokana na ustadi wake wa kung'amua maana ya neno katika muktadha fulani na katika utamaduni wake na hii imemwezesha kupata viwakilishi mwafaka katika L.L. Watafiti wanaendelea kusema kuwa tafsiri hii imefanikiwa katika viwango vifuatavyo vilivyopendekezwa na Newmark (1988): umakala unaohusu kubadilisha sarufi ya L.A kwenda kwa L.L; ni kupata viwakilishi vya L.A katika L.L na vilevile kutafsiri msamiati kwa ajili ya kukubalika katika muktadha wa sentensi.

Watafiti wanakiri kwamba mtafsiri amemudu umakala kwa kiwango kikubwa. Udhaifu uliodhihirika ni mdogo sana ukilinganishwa na ufaafu. Kiwango kingine ni mshikamano ambao hutokea kupitia matumizi sahihi ya viunganishi, vionyeshi, vibainishi, msamiati wakilishi, msamiati jumuishi na uakifishaji sahihi ili kuunganisha sentensi. Mshikamano huu umejitokeza katika M.L kwa vile sentensi zake zinatiririka na kuambatana vyema na za M.A na hivyo kueleweka na hadhira ya M.L. Uaminifu ni kiwango kingine na unahusu mtafsiri kujua uamilifu

wa M.A na maana na atafsiri bila kuongeza au kutoa maana nyingine. Licha ya kuwa na hitilafu chache katika tafsiri hii, mtafsiri amedhihirisha kuelewa uamilifu wa M.A ambao ni kusifu na kuomba na amejikakamua kuuhifadhi katika M.L . Tafsiri hii ina kiwango kingine pia kilichopendekezwa na Newmark ambacho ni ukawaida. Ukawaida ni kule kuhakikisha tafsiri ina fahiwati, ni yenye lugha sahili na haina mbwembwe. Kufuatwa kwa viwango hivi vyote kunadhihirisha kuwa tafsiri imefaulu.

Watafiti wanadai kuwa kiwango cha urejeleaji hakikutimizwa ifaavyo na mtafsiri. Urejeleaji unahusu kurejelea M.A mara kwa mara ili tafsiri isipotoke. Wanadai kuwa mtafsiri angezingatia urejeleaji, angegundua hitilafu chache walizogundua. Hata hivyo, wanakiri kuwa hakuna tafsiri iliyo kamili na kuona hii kama iliyofanikiwa kwa vile inatimiza usawa wa kikazi unaopendekezwa na House (2015). Fauka ya hayo, watafiti wanadai kuwa tafsiri ya ombi hili imefanya kazi ya kuwa daraja la kitamaduni linalotajwa na House (2015) na kuwezesha kupatikana kwa habari kwa usawa katika ulimwengu huu wa uwingi lugha. Hili ni jukumu la tafsiri lililotajwa hapo awali na Cronin (2013). Aidha, limewezesha uhifadhi na usambazaji wa utamaduni na fasihi, jukumu lililotajwa na Venuti (2012). Mafanikio haya yote yametokana na kufaulu kwa tafsiri ya ombi hili.

Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imehakiki ufaafu wa tafsiri ya ombi la *Baba Yetu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Imeanza kwa kutoa fasiri tofauti za neno tafsiri, ikaonyesha umuhimu wa tafsiri na pia kuonyesha uwezo na stadi tofauti zinazohitajika na mtafsiri na msomaji katika mchakato wa kutafsiri na kufasiri. Uhakiki wa tafsiri ya ombi la *Baba Yetu* unadhihirisha kuwa tafsiri hii imefanikiwa kwa vile imefuata viwango vilivyopendekezwa na Newmark na vilevile mkabala wa House wa tafsiri kuhusu ubora wa tafsiri. Tafsiri hii imetimiza usawa wa kikazi unaopendekezwa na House na vilevile kimawasiliano inavyopendekezwa na Newmark. Wanapendekeza kuwa katika mapitio yajayo, udhaifu uliogunduliwa uangaliwe upya ili kuboresha tafsiri hii zaidi.Watafiti wanaenzi taaluma ya tafsiri kwa vile ni daraja la mawasiliano kati ya jamii tofauti zenye tamaduni tofauti. Wanatumai kuwa makala hii itachangia pakubwa kwa wasomi wa kazi ya tafsiri kwa vile wataitumia kujenga malengo ya tafiti zao na kuimarisha tafiti zao kwa kuitumia kama rejeleo la kazi zao. Pamoja na hayo, watafiti wanapendekeza, kwa vile tuko katika kipindi cha kidijitali, watafiti wa baadaye wanaweza kutafiti kuhusu ufaafu wa tafsiri zilizofanywa kidijitali.

Marejeleo

Bible Society of Kenya (1997). *Biblia Maandiko Matakatifu.* Bible Societies of Kenya & Tanzania.

Cartford, J.C. (1965) *A Linguistic Theory of Translation*. Oxford University Press.

Cronin, M. (2013). *Translation in the Digital Age*. Routledge.

Erton, I. (2020). Linguistic and Cognitive Aspects of Translation and Interpretation Skills. *Journal of Languages and Linguistic Studies*, 16(4), 1910-1920.

Food and Agriculture Organization. (2021). *Africa regional overview of food security and nutrition 2021*. FAO. https://www.fao.org/publications/card/en/c/CB7495EN/

Franzon, J. (2008). Choices in song translation: Singability in print, subtitles and sung performance. *The Translator*, 14(2), 373–399.

House, J. (2015). *Translation Quality Assessment: Past and Present*. Routledge.

House, J. (1977). *A Model for Translation Quality Assessment.* Gunter Narr Verlag https://mukuyu.wordpress.com

Low, P. (2013). When songs cross language borders: Translations, adaptations and 'replacement texts'. *The Translator*, 19(2), 229–244.
Metzger, B. M., & Ehrman, B. D. (2005). *The Text of the New Testament: Its Transmission,Corruption, and Restoration* (4th ed.). Oxford University Press.
Munday, J. (2016). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications* (4th ed.). Routledge.
Newmark, P. (1988). *A Textbook on Translation*. Prentice Hall
Nida, E. na Taber, C.R. (1992). *The Theory and Practice of Translation.* Netherlands Printing Press
Pelikan, J. (2005). *Whose Bible Is It?: A History of the Scriptures Through the Ages*. Viking.
Pym, A. (2010). *Exploring Translation Theories*. Routledge.
Spencer, C. (2002). *British food: An extraordinary thousand years of history*. Grub Street Publishing.
The Holy Bible- New King James Version (1982).
Venuti, L. (2012). *The Translator's Invisibility: A History of Translation*. Routledge.

Kiambatisho

Our Father which art in heaven, Hallowed be thy name. Thy kingdom come. Thy will be done on earth, *as it is* in heaven. Give us this day our daily bread. And forgive us our debts, as we forgive our debtors. And lead us not into temptation, but deliver us from evil: For thine is the kingdom, and the power, and the glory, for ever. Amen (Matthew 6:9-12).
(*The Holy Bible- King James Version*)

Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamahevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina (Mathayo 6:9-12)
(*Biblia Maandiko Matakati*